GAZETI LA SERIKALI Na. 577 la tarehe 11/8/2023

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272*)*

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 29 (1) (d))*

AMRI ZA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA DODOMA ("DODOMA WSSA"), YA YA MWAKA 2023

Kichwa cha Agizo

1. Amri hiziI zitajulikana kama Amri za Kurekebisha Bei za Huduma za Maji za Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Dodoma ("Dodoma WSSA"), ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya B

2. Bei za maji safi na usafi wa mazingira za Dodoma WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa katika Amri hii zitaambatana na masharti yafuatayo;

(a) Mnamo au kabla ya tarehe 30 Septemba 2023, Dodoma WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hili;
(b) Mnamo au kabla ya tarehe 30 Septemba 2023, Dodoma WSSA itawasilisha EWURA mkataba wa huduma kwa mteja uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na viwango vya huduma vilivyooneshwa kwenye mpango biashara;
(c) Dodoma WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika

Jedwali la Pili la Amri hili.

(d) Kabla ya kutoa ankara kwa mara ya kwanza kwa ajili ya matumizi ya bei na ada zilizoainishwa kwenye Amri hili, Dodoma WSSA itawasilisha ushahidi kwa EWURA kuwa iliwaarifu wateja wake na kutoa elimu ya kutosha kwa wadau wake kama vile viongozi wa serikali na vyama vya siasa, viongozi wa dini, wateja wake na wadau wengine, kuhusu mabadiliko ya bei za huduma zake;

(e) Dodoma WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu;

(f) Dodoma WSSA kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne;

(g) Katika kuhakikisha kunakuwepo na huduma endelevu ya maji hususan kipindi cha kiangazi, Dodoma WSSA inaelekezwa kuandaa na kutekeleza mpango wa kuvuna maji ya mvua;

(h) Ifikapo 30 June 2026 Dodoma WSSA itafanya ukaguzi wa utekelezaji wa Mpango wa biashara na Mkataba wa huduma kwa wateja wake kama inavyohitajika kwenye Kanuni za Utoaji Leseni na Ubora wa Huduma za Mwaka 2020 na kuwasilisha taarifa EWURA; na

(i) Dodoma WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Dodoma WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na

uboreshaji wa huduma zake.

TS.Na. 425 la 2019

4. Amri hii inafuta Amri ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Matumizi | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Matumizi 1 (0-5) | 1,170 | 1,510 | 1,650 | 1,858 |
| | Matiumizi 2 (Juu ya 5) | 1,300 | | | |
| Taasisi | | 1,620 | 1,880 | 2,050 | 2,316 |
| Biashara | | 1,660 | 1,930 | 2,100 | 2,373 |
| Viwanda | | 1,660 | 1,930 | 2,100 | 2,373 |
| Maghati | | 600 | 1,000 | 1,500 | 1,500 |
| Wateja Wakubwa | | 1,800 | 2,000 | 2,060 | 2,100 |
| Wastani Wa Bei | | 1,400 | 1,627 | 1,777 | 2,001 |
| Watani wa Bei zilizokokotolewa | | | 1,628 | 1,774 | 2,001 |

Jedwali Namba 1(b): Bei ya Sasa na Zilizoidhinishwa ya Uunganishaji Mpya wa Maji na Majitaka (Tshs /Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |

*Tangazo la Serikali Na.577 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Majumbani | Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Taasisi | | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Biashara | | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Viwanda | | 26,000 | 26,000 | 26,000 |

Jedwali Namba 1(c): Bei ya Sasa ya na Zilizoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji (Tshs/ Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 15,000 | 25,000 | 25,000 | 25,000 |
| Taasisi | 15,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Biashara | 15,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Viwanda | 15,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Magati | 15,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |

Jedwali Namba 1(d): Bei za Maji Taka za Sasa na Zilizoidhinishwa (Tshs/m3)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Asilimia 40 ya Usambazaji Maji (Metered Water) | Asilimia 40 ya Usambazaji Maji (Metered Water) | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

Jedwali Namba 1(e): Bei za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kuondoa Majitaka (Tshs/Safari 6m3)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 60,000 | 100,000 | 120,000 | 140,000 |
| Zisizo za Majumbani | 75,000 | 115,000 | 130,000 | 145,000 |

Jedwali Namba 1(f): Bei za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kuondoa Maji Taka (Tshs/m3)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Umwagaji wa Maji Taka | 1,000 | 1,000 | 1,250 | 1,500 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya 3(c))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA (KIASI SHILINGI MILIONI)

| Na. | Maelezo ya Mradi | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uchimbaji na ufungaji wa Pampu 10-kwa mwaka zenye uwezo kuanzia 20m3/saa, Casings za DN 150mm. excavation and backfilling of trenches within and off-grid area | 1,731.39 | 1,923.70 | 2,266.97 |
| 2 | Ununuzi wa GPS 8, simu 48 na programu ya GIS | 35.00 | 5.00 | 5.00 |
| 3 | Ununuzi wa DN 15 mita za maji za malipo ya kabla daraja C (8,400 pcs kwa mwaka) | 1,050.00 | 1,050.00 | 1,050.00 |
| 4 | Ubadilishaji wa mita za maji 6,000 chini ya usajili kwa kufunga mita za maji daraja C za DN 15mm. (mita 4,936 mwaka 2023/24 na mita 3,040 mwaka 2024/25 na mita 3,040 kwa mwaka 2025/26) | 617.00 | 380.00 | 380.00 |
| 5 | Ununuzi wa zana za kufanyia kazi (Gari 1- CC 2400 double cabin (mwaka wa pili), Pikipiki 12 kila mwaka12, welding machines, Pampu za kumwagilia, Spana toolbox, fimbo kwa ajili ya kuzibua maji taka) | 142.00 | 155.00 | 180.00 |

*Tangazo la Serikali Na.577 (Linaendelea.)*

| Na. | Maelezo ya Mradi | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Upanuzi wa mabomba ya maji PN 10, DN 75mm to 150mm kwenye maeneo mapya ya Nzuguni 8.5, Mkonze 5.3, Miganga 4.5, Ilazo Extension 3.6, Ndachi 4.2, Kikuyu 4.7, Mkonze 5.3, Mipango 3.3, Miyuji 7.7 Mapinduzi 5.0, Kinyambwa Extension 4.6, Msalato 3.0, Ntyuka 2.7, Mpamaa 3.4, Swaswa 4.0, Msangalale/Njedengwa 2.9, Chidachi 2.5, Mkalama 1.0, Ihumwa 5.3, Iyumbu 3.1, Mbwanga 2.1, Nala 4, Michese 3.7, Kongwa 15km, Bahi 20km, Chamwino, 20km, Kibaigwa 24km kwa ajili ya kuunga wateja 2,100 kwa urefu wa km 40 kwa mwaka 2023/24, km 53 kwa mwaka 2024/25, na km 87 kwa mwaka 2025/26 | 2,047.00 | 2,673.85 | 4,389.15 |
| 7 | Ukarabati miundombinu chakavu ya maji km 96 maeneo ya Mji mpya km 6, Kikuyu Kaskazini km1 Miyuji, Mpamaa & Mlimwa C km23, Kongwa km23, Bahi km3, Chamwino km 5, Kibaigwa km13, Mkalama km 6, Msalato km 3, Madukani km5, Majengo km2, Image km3, na NHC Iringa Road km3 kwa mabomba ya ujazo wa DN 63mm - DN 160mm, PN 10 kwenda umbali wa km 18 mwaka 2023/24, km 39 mwaka 2024/25, na km 39 mwaka 2025/26. | 950.19 | 2,000.00 | 2,000.00 |
| 8 | Ukarabati wa mabomba ya maji taka kwa jumla ya urefu wa km 2.5. Bahiroad km 0.8, Area A km 0.7), Uhindini km 0.5, Makole km 0.4 na Mjini kati 0.4km kwa mabomba yenye upana kuanzia DN 100mm - DN 160mm, PN 6 kwenda urefu wa km1 mwaka 2024/25, na km 1.5km kwa mwaka 2025/26 | - | 257.90 | 386.84 |
| | Jumla | 6,572.58 | 8,445.44 | 10,657.96 |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3 (e))*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Maelezo | Kizio | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Asilimia ya Idadi ya watu inayofikiwa na huduma ya maji | % | 85 | 90 | 95 |
| Maunganisho mapya ya majisafi | No. | 8,400 | 8,400 | 8,400 |
| Maunganisho mapya ya majisafi | No. | 216 | 216 | 1,000 |
| Upotevu wa Maji | % | 27 | 26 | 25 |
| Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja | % | 100 | 100 | 100 |
| Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato | % | 98 | 98 | 98 |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(f))*

MAPATO YANAYOHITAJIKA

| Marekebisho ya Mahitaji ya Mapato (Tshs "000") | | | |
|---|---|---|---|
| Maelezo | Makisio | | |
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Gharama za Uzalishaji | 8,632,789 | 9,230,635 | 10,889,108 |
| Gharama za Usambazaji | 7,872,673 | 8,921,344 | 10,794,827 |
| Gharama za huduma ya Mati Taka | 541,764 | 655,534 | 793,196 |
| Gharama za Kiiutumishi | 7,108,628 | 7,317,853 | 7,645,693 |
| Gharama za Kiutawala | 4,206,917 | 4,315,691 | 4,473,450 |
| Gharama za Matangazo | 544,679 | 568,372 | 593,835 |
| Gharama za Matukio na Ufadhili | 51,233 | 60,425 | 61,670 |
| Gharama za Bodi | 145,900 | 152,291 | 158,961 |
| Gharama za Utunzaji wa Fedha | 47,597 | 457,385 | 51,858 |
| Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo | 29,152,180 | 31,679,530 | 35,462,598 |
| *Return on Investment* | 1,059,491 | 740,464 | 614,598 |

*Tangazo la Serikali Na.577 (Linaendelea.)*

| Marekebisho ya Mahitaji ya Mapato (Tshs "000") | | | |
|---|---|---|---|
| Maelezo | Makisio | | |
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Uchakavu | 8,318,443 | 11,881,550 | 16,437,714 |
| Mapato Yote Yanayohitajika | 38,530,114 | 44,301,544 | 52,514,910 |
| Ondoa: | | | |
| Mapato mengineyo | 6,238,098 | 6,865,961 | 7,559,087 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Maji | 32,292,016 | 37,435,583 | 44,955,823 |

Dodoma,
.............................,2023

JAMES A MWAINYEKULE,
*Mkurugenzi Mkuu*